

A- صِفَاتُ ذَوَاتِ الْأَصْدَادِ Swifaatu dhawaatil-adhwaad - Swiffah zilizo na kinyume

1. Al-Hams - Kunong'ona¹ اَلْهَمْسُ na kinyume chake ni Al-Jahr - Kusikika اَلْجَهْرُ; Swiffah hizi zina athari ya sauti.

<p>اَلْهَمْسُ Al-Hams (Kunong'ona)</p>	<p>اَلْجَهْرُ Al-Jahr (Kusikika)</p>
<p>Kutoa pumzi yaani sauti ya kunong'ona inayotoa upepo wakati wa kutamkwa herufi katika herufi za al-hams. Herufi zake ni kumi (10) zimekusanywa katika ibara:</p> <p>فَحْتَهُ شَخْصٌ سَكَّتْ</p> <p>Ukiweka mkono mbele ya mdomo ukatamka herufi hizi, utahisi hewa kutoka mdomoni. Jaribu kutamka herufi zifuatazo:</p> <p>أَفْ فَ فُ فِ</p>	<p>Kuzuia kutoka pumzi yaani kutokutoa sauti ya kunong'ona wakati wa kutamkwa herufi. Herufi ni zilizobakia ukizitoa herufi zisizokuwa za al-hams.</p> <p>أ ب ج د ذ ر ز ض ط ظ ع غ ق ل م ن و ي</p>

¹ Kutokana na upana wa lugha ya Kiarabu, maana za Swiffah huenda zikawa si kama zilivyokusudiwa lakini nimejaribu kuzipa maana za karibu kabisa, na itahitaji mwalimu kufafanua zaidi.

2. الشِّدَّة Ash-Shiddah -Nguvu na kinyume chake ni الرَّخَاوَة Ar-Rakhaawah - Udhaifu na baina yao iko At-Tawassutw - التَّوَسُّط - Wastani.

الشِّدَّة Ash-Shiddah (Nguvu)	التَّوَسُّط At-Tawassutw (Wastani)	الرَّخَاوَة Ar-Rakhaawah (Dhaifu)
<p>Kuzuia kutoka kwa sauti wakati wa kutamkwa herufi miongoni mwa herufi za ash-shiddah. Mfano ت خُلِقَتْ katika</p> <p>Herufi zake ni nane (8) zimekusanywa katika ibara:</p> <p>أَجْدُ قَطٍ بَكْتٌ</p>	<p>Swiffah iliyopo baina ya ash-shiddah na ar-rakhaawah kwa maana; sauti haizuiliki kikamilifu wala haiendelei kikamilifu bali huwa kati na kati.</p> <p>Herufi zake ni 5 zilizokusanywa katika ibara:</p> <p>لِنْ عُمَر</p>	<p>Kutangulia kutoka sauti wakati wa kutamka herufi miongoni mwa herufi za ar-rakhaawah. Mfano ش katika مَعَايِش</p> <p>Herufi zake ni zote zilobakia ukitoa herufi za ash-shiddah na at-tawassutw</p> <p>ث ح خ ذ ز س ش ص ض ظ غ ف و ه ي</p>

3. الإطباق Al-Itwbaaq – Kufunga na kinyume chake ni الإنفتاح Al-Infitaah
- Kufungua; Swiffah hizi zina athari ya sauti

<p>الإطباق Al-Itwbaaq (Kufunga)</p>	<p>الإنفتاح Al-Infitaah (Kufungua)</p>
<p>Kukutana sehemu ya ulimi na sakafu ya juu ya mdomo (kufungika) wakati wa kutamka herufi. Swiffah hii huilazimu herufi kufungika hata ikiwa ina <i>i'raab</i> ya kasrah. Herufi zake ni nne (4) zenye nguvu kabisa.</p> <p style="text-align: right;">ص ض ط ظ</p>	<p>Kutenganisha baina ya ulimi na sakafu ya juu ya mdomo wakati wa kutamka herufi na hivyo mdomo hufunguka. Herufi zake ni herufi zote zisizokuwa za al-itwbaaq</p> <p style="text-align: right;">أ ب ت ث ج ح خ د ذ ر ز س ش ع غ ف ق ك ل م ن و ه ي</p>

4. الإِسْتِغْلَاءُ Al-Isti'-laa - Kupaa juu na kinyume chake ni الإِسْتِيفَالُ Al-Istifaal - Kuinamisha² Hizi ni swiffah za lazima ambazo haziepakani na dhati ya herufi. Swiffah hizi zina athari ya sauti

<p>الإِسْتِغْلَاءُ Al-Isti'-laa (Kupaa juu)</p>	<p>الإِسْتِيفَالُ Al-Istifaal (Kuinamisha)</p>
<p>Kuelekeza shinikizo ya herufi (hewa yake) kwa kupandisha ulimi juu ya sakafu ya mdomo wakati wa kuitamka herufi na kujaza mdomo. Herufi zake ni saba (7) zilizokusanywa katika ibara:</p> <p style="text-align: center;">خُصَّ صَغَطِ قِطْ</p>	<p>Kuteremsha ulimi chini wakati wa kutamka herufi yaani kutokufanya mdomo kujaa. Herufi zake ni herufi zote zisizokuwa za الإِسْتِغْلَاءُ (al-isti'laa).</p> <p style="text-align: center;">أ ب ت ث ج ح د ذ ر ز س ش ع ف ك ل م ن و ه ي</p>

²Inajulikana pia kama ni Tafkhiym na Tarqiyq - Tafkhiym na Tarqiyq ni matokeo ya Swiffah ya الإِسْتِغْلَاءُ (al-isti'laa) na الإِسْتِيفَالُ (al-istifaal), hivyo Tafkhiym na Tarqiyq ni Swiffah "Aaridhwah" za kuzuka.

5. الإذلاق Al-Idhlaaq – Mtiririko na kinyume chake ni الإصمات Al-Iswmaat – Kuzuilika; swiffah hizi hazina athari ya sauti³

<p>الإذلاق Al-Idhlaaq (Wepesi na uharaka)</p>	<p>الإصمات Al-Iswmaat (Kuzuilika/Uzito na ugumu)</p>
<p>Wepesi na uharaka wa kutamka herufi kwa sababu ya kutoka kwake kutoka ncha ya ulimi au midomo miwili. Imeitwa hivyo kwa kuwa baadhi yake hutoka ukingoni mwa ulimi, nazo ni: ر ن ل na baadhi yake hutoka kutoka midomo miwili, nazo ni: ف م ب Herufi zake zimekusanyika katika ibara: فَرَّ مِنْ لُبِّ</p>	<p>Kuhitajika juhudi ya kuzitamka herufi na hutamkwa polepole na kutoka ndani ya mdomo na koo. Herufi zake ni herufi zote zisizokuwa za al-idhlaaq أ ت ث ج ح خ د ذ ز س ش ص ض ط ظ ع غ ق ك و ه ي</p>

Tanbihi: Swiffah hizo zote zinakuwa na nguvu zaidi herufi zinapokuwa zina sukuwn, na zinapunguka zinapokuwa na *i'raab*.

³ Zinahusiana na Swarf katika lugha ya Kiarabu.